

## **MWONGOZO WA VIAMBATA VINAVYOHITAJIKA KWENYE UJAZAJI WA FOMU ZA MALIMBIKIZO YA MISHAHARA.**

### **A: MADAI YANAYOHUSIANA NA KUPANDA/KUBADILISHIWA CHEO (PROMOTION)**

Kwa Mtumishi ambaye alipandishwa au alibadilishiwa cheo na mshahara wake ulirekebishwa kwa kuchelewa anapaswa kuambatisha nyaraka zifuatazo:-

- Nakala ya Barua ya kupandishwa cheo/Kubadilishiwa cheo
- Nakala ya risiti za mishahara (Salary Slip) ya mwisho kupokea mapunjo na ya kwanza ya mshahara mpya.

***Mfano: kama ulipandishwa cheo mwezi Oktoba, 2014 mshahara ukarekebishwa mwezi Machi, 2015 utatakiwa uwasilishe salary slip za mwezi Februari, 2015 na Machi, 2015.***

- Barua ya Maombi ya kulipwa Madai ya Malimbikizo ya Mishahara (iandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) kupitia kwa Mkuu wa Idara husika). Iainishe muda wa deni (toka mwezi gani hadi mwezi gani) na kiasi kinachodaiwa.

### **B: MADAI YANAYOHUSIANA NA AJIRA MPYA**

Kwa Mtumishi ambaye aliajiriwa lakini alichelewa kuingizwa kwenye Payroll anapaswa kuambatisha nyara zifuatazo:-

- Nakala ya barua ya ajira
- Nakala ya salary slip ya kwanza baada ya kuingizwa kwenye payroll
- Barua ya Maombi ya kulipwa Madai ya Malimbikizo ya Mishahara (iandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) kupitia kwa Mkuu wa Idara husika). Iainishe muda wa deni (toka mwezi gani hadi mwezi gani) na kiasi kinachodaiwa

### **C: MADAI YANAYOHUSIANA NA KUONDOLEWA KWENYE PAYROLL (DQ, TM, SN....)**

Kwa Mtumishi ambaye aliondolewa kwenye payroll kwa sababu mbalimbali lakini baada ya ufuatiliaji kufanyika alirejeshwa kwenye payroll anapaswa kuambatisha nyaraka zifuatazo:-

- Nakala ya salary slip ya mwisho kabla ya kuondolewa kwenye payroll
- Nakala ya salary slip ya kwanza baada ya kurejeshwa kwenye payroll
- Barua ya Maombi ya kulipwa Madai ya Malimbikizo ya Mishahara (iandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) kupitia kwa Mkuu wa Idara husika). Iainishe muda wa deni (toka mwezi gani hadi mwezi gani) na kiasi kinachodaiwa,
- Barua yeyote inayotoa maelezo yanayohusiana na kukosa mishahara hiyo (kama ipo)

**NB: Viambatisho vinapaswa kuonekana ili visilete usumbufu kwenye rejea.**